# Learning by Ear – Religious Dialogue: "A Bridge over Gori"

## Episode 04: "Chini ya Daraja la Gori"

**Author: Romie Singh**

**Editors: Katrin Ogunsade, Naïma Guira**

**Proof reading: Natalie Glanville-Wallis**

**Expert on African religions: Jean-Félix Belinga Belinga**

**KISUAHELI ERIC PONDA**

**List of characters for episode 4:**

- Narrator /Philip, male (17)
- Harry, male (17)
- Layla, female (16)
- Roshi, female (16)
- School Director, Mrs Ayo Milulu, female (48)
- Hassan (Layla's brother) (12)
- + Students in the background

**1. SIG TUNE UP**

**2. INTRO:**

**Hujambo msikilizaji na karibu kwa sehemu ya nne ya mfululizo wa mchezo huu wa Redio DARAJA LA MTO GORI,hadithi inayoelezea jinsi Dini na Siasa zinavyoweza kuzua uhasama kati ya Jamii mbili kadhalika familia mbili za Mzee Dembele na Omer. Katika kipindi hiki "CHINI YA DARAJA" Harry Dembele na Layla Omer ,viranja katika shule ya Ubuntu, wamegundua kuwa kundi la mjadala na mdahalo huenda likayabadili maisha ya wanafunzi wengine kwa kiasi kikubwa. Philip ni mmoja ya marafiki wa dhati wa Harry.Yeye ndiye msimulizi wa makala hii.Usiondoke!**

**Scene 1. In Ubuntu college**

**Director**

**3. Atmo: School, morning Assembly - INSERT UBUNTU ANTHEM (ending)**

**4. DIRECTOR:** **Ahsanteni sana wanafunzi wapendwa kwa kuimba vizuri.Ningependa kuwahimiza kuwa adilifu kwa kila jambo mnalolifanya. Bila shaka ni vizuri kutuzwa kila unapofanya kazi vizuri.Hata hivyo hatupaswi kuwa waadilifu kwa madhumuni ya kutarajia tuzo la aina Fulani-iwe ni ahera,wadhifa muhimu au nishani. La hasha,kila jambo tunalojaribu na tunalofanikiwa liwe kwa uwezo wako wote.Tuzo yenyewe ni kujua kuwa umeiridhisha nafsi yako.Hisia hiyo ni muhimu zaidi hasa ukitanabahi kuwa ulilolifanya lina manufaa kwa wengine pia.Huo ndio msingi wa Chuo cha Ubuntu. Sasa nawaomba muelekee madarasani mwenu na nawatakia siku iliyojawa na fanaka.**

**5. SFX: STUDENTS WALK OUT/TALKING/MURMURING / FADE OUT**

6. **PHILIP/NARRATOR: Ni mwanzo wa siku nyingine shuleni baada ya wikendi,iliyokuwa na mafanikio machache.Harry alikuwa amevunjika moyo baada ya safari yake ya kumtembelea babake kijijini.Tulikuwa tunajaribu kumchangamsha wakati Layla alipoingia. Kwani hata alinitazama?!, Wala hakunitia shughuli, alitaka tu kuzungumza na Harry …..peke yao..!.**

**<u>Scene 2. School gardens</u>**

**Harry, Layla**

7. **<u>SFX: School gardens: students playing, talking in the background, birds</u>**

8. **LAYLA:** **Harry ….uko sawa.?**

9. **HARRY:** ***(snappy)*** **Ehh niko sawa Layla..!.**

10. **LAYLA:** **Nakuona leo huna furaha…. Nilitaka tu kukufahamisha kwamba Mkurugenzi anataka tukutane mwendo wa saa sita hivi kwenye maktaba. Anataka tuzungumze kuhusu suala la uzinduzi wa kundi la mjadala utakaofanyika siku ya Alhamisi.**

**11. HARRY:** **Sawa,…. ila samahani Layla, kama unaniona nimebadilika.. Ni kwasababu ya Babangu mdogo…! Tunaweza kuzungumza kwa muda mchache tu Layla.. sio hapa lakini … baadaye huko nje….!?**

**12. LAYLA:** **Lakini unaonekana huna furaha kabisa ,…. Nataraji si jambo baya,ama?**

**13. HARRY:** **Wacha tutazungumza baadaye Layla….! Je tunaweza kukutana chini ya Daraja baada ya masomo?**

**14. LAYLA:** **Kawaida mdogo wangu Hassan hufika hapa mwendo wa saa tisa kunichukua twende nyumbani.**

**15. HARRY:** **Sawa …..nitakupeleka nyumbani kama atakubali.. sawa?**

**16. LAYLA:** ***(uncertain)* Sawa , sawa *(happier)* ni sawa hakuna neno!!**

**17. HARRY:** **Sawa basi.. tukutane baadaye mwendo wa saa sita kwenye maktaba**

**18. LAYLA:** **Sawa baadaye basi!**

**19. BRIDGING MUSIC**

**Scene 3. On the sports field**

**Roshi, Layla, students in the background**

**20. SFX: birds, people shouting and laughing, voices in the background, people running in the background, playing basketball**

**21. ROSHI:** **Kwanini unanitazama na macho hayo ya kung'ara hivyo Layla?**

**22. LAYLA:** **Uuuhhh,Roshi tafadhali** ***(Laughing)*** **Yaani wewe hupitwi na chochote!!**

**23. ROSHI:** **Haha! Kwa hivyo liko jambo.. ! Ehhh niambie mwenzangu..! ni…. Ehhh, Philip Layton Browne amekualika mtoke ?**

**24. LAYLA:** **Eti nini? Wacha upuzi wako!**

**25. ROSHI:** **Sawa… basi labda ..ehhh ….Unampenda Harry Dembele!..., sivyo?**

| | | |
|---|---|---|
| **26.** | **LAYLA:** | **Roshi! Tosha sasa…! Hao wote tunashirikiana kikazi. Nitawezaje kufanya kazi yangu vizuri kama kiranja, iwapo utanishuku kwa kila jambo?** |
| **27.** | **ROSHI:** | **Kila jambo unalofanya? ….Ehh kumbe mambo yamebadilika… unanifurahisha…!** |
| **28.** | **LAYLA:** | **Komea papo hapo, umeanza kubadili kauli zangu…! Tafadhali ifunge fundo hii Hijabu yangu huko nyuma sije nywele zikanifika uso nikikimbia.** |
| **29.** | **ROSHI:** | ***(singing softly)*** **Layla ameanza uhusiano wa kimapenzi… mahaba..heee! Layla ameanza Mapenzi ?.** |
| **30.** | **LAYLA:** | **Ouch! Mbona wanivuta nywele?** |
| **31.** | **ROSHI:** | **Oooh – Pole…...** |
| **32.** | **LAYLA:** | **Tufanye mazoezi kidogo kisha tukimbie.** |
| **33.** | **ROSHI:** | ***(panting while warming up)*** **Sawa ….! Lakini nadhani sijakosea kuhusu Philip. Anakuandama kama kondoo!** |

**34. LAYLA AND ROSHI:** **(<u>Counting 1 and 2 and 3.. as they exercise)</u>**

**35. <u>BRIDGING MUSIC UP AND FADE</u>**

**<u>Scene 4. In the library</u>**

**Director, Harry, Layla, students in the background**

**36. <u>SFX: students murmuring softly in the background, rustling of paper in the background</u>**

**37. DIRECTOR:** **Tayari mumefika. Twendeni pale pembeni ili tuweze kujadiliana. Ehh wikendi yenu ya kwanza ilikuwaje?**

**38. HARRY+ LAYLA:** **Ilikuwa nzuri Bi Milulu**.

**39. <u>SFX: rustling of book pages, closing books with a snap, standing up from chairs, footsteps</u>**

**40. LAYLA:** **Tulijaribu kuwaulizia wanafunzi wengine kuhusu maada wanazotaka kuzijadili tutakapoanzisha mijadala.**

**41. HARRY:** **Na tukazungumza na wanafunzi wa mwaka wa kwanza na wapili … wote… wasichana kwa wavulana….kuhusu maada hizo!**

**42. DIRECTOR:** **Baada ya hapo?**

***43.*** **HARRY:** **Maada iliyopewa umuhimu zaidi ni Ndoa za wake wengi, yaani Ndoa ya *Mitala..!***

**44. DIRECTOR:** **Hmm, …. Hilo halinishangazi!.Suala hilo limetangazwa kwenye vyombo vya habari kwa muda tangu waziri wetu wa Afya alipooa mke wa tano!**

**45. LAYLA:** **Ndilo suala lenyewe hilo:Jee anatoa mfano mzuri tukizingatia enzi hii ya Ugonjwa wa Ukimwi na virusi vya HIV?**

**46. DIRECTOR:** **Ni kweli… Kwanza mada hiyo inatupa mwelekeo mzuri.**

**47. LAYLA:** **Na maada ya pili iliyopewa uzito ni, Iwapo Shule ya Ubuntu inafanya juhudi za kutosha kuwaunga mkono wanafunzi wa kike kushiriki katika michezo.**

**48. DIRECTOR:** **Ooooh! Bila shaka wasichana ndio waliochangia mada hiyo!**

**49. LAYLA:** **Ndiyo.Sheria za Kiislamu zinawalazimu wasichana wajistiri .Tayari mwalimu wa michezo ametangaza kwamba hataruhusu *Hijab* na mavazi marefu kwasababu si mavazi rasmi ya michezo..**

**50. HARRY:** **Huo ndio uamuzi uliotolewa na kamati ya michezo katika eneo hili.**

**51. LAYLA:** **Kwa kweli , Hata wavulana wa Kiislamu hawapaswi kuonyesha sehemu zao za miguuu, au mikono, lakini ni wasichana tu wanaotatizika kwani lazima wafunike na vichwa vyao pia.Hilo haliwahusu wanafunzi wa kiume...!**

**52. DIRECTOR:** **Hmm… Nadhani itakuwa bora tukilitathmini suala hilo na kuliwasilisha kwa kamati ya michezo ili liweze kujadiliwa upya.**

**53. LAYLA:** **Bi Milulu labda tunaweza kuuliza , "Je unadhani sheria kuhusu mavazi zinapaswa kubadilishwa ili wanafunzi wote wa kiislamu waweze kushiriki katika michezo bila vikwazo?"**

**54. DIRECTOR:** **Bila shaka nitaliwasilisha kwa bodi ya shule ..Tayari mumepata mada muhimu za kujadili!Kumbukeni kuna shindano la mjadala lililopangwa kufanyika hapa Gori baadaye mwaka huu na kauli mbiu yake ni "Jieleze vizuri,Zungumza waziwazi".Tunahitaji kujiandaa kwa hilo pia.Sasa nawaacha mukauandae ufunguzi rasmi wa Kundi la kwanza la mjadala na mdahalo la Chuo cha Ubuntu.Kila la Kheri!.**

**55. HARRY/LAYLA:** **Ahsante na kwaheri..**

**56. SFX: Footsteps leaving on cement or stone floor. Door opens/closes**

**57. HARRY:** **Mimi pia naondoka.Uwe kwenye lango kuu la shule mwendo wa saa tisa kamili! Tuonane baadaye** ***(off mic)*****Nataka kukutana na Hassan!**

**58. LAYLA:** ***(Softly to herself)*** **Hmm… Jambo la kufurahisha sana hilo!**

**59. BRIDGING MUSIC**

**<u>Scene 5. At the main gates</u>**

**Layla, Harry, Hassan, students in the background**

**60. <u>SFX: birds, students' voices, students passing by, traffic in the distance</u>**

**61. LAYLA:** **Hassan, huyu ni Harry Kiranja wetu wa kiume shuleni ..**

**62. HARRY:** **Nashkuru kufahamiana nawe Hassan**

**(Silence)**

**63. HASSAN:** **Habari yako Harry..? Layla njoo twende**

**64. LAYLA:** **Hassan,usiwe mjeuri. Mimi na Hassan tunahitaji kukutana kwa muda wa nusu saa hivi.**

**65. HASSAN:** **Eti nini? Nyinyi peke yenu?**

**66. HARRY:** **Um...Sikiza hapa Hassan..! Hatutachukua muda mrefu. Je naweza kumleta Dadako Nyumbani, baada ya saa moja hivi?**

**67. HASSAN:** **Nitaandamana na nyinyi .**

**68. LAYLA:** **Hassan, hapana tafadhali nenda Nyumbani Nitakuja nyumbani pindi nikimaliza.**

**69. <u>Hassan clicks his tongue. Layla sighs. Footsteps fade</u>**

**70. HARRY:** **Samahani nataraji sijamkasirisha.**

**71. LAYLA:** **Amekasirika lakini.. si wewe peke yako , siku hizi anamkasirikia kila Mtu. Harry lakini tusikawie..!. Babangu hayuko nyumbani na siwezi kumuacha Hassan peke yake nyumbani. Nadhani kifo cha mama bado kinamsumbua sana .**

**72. <u>SOFT LOW DRAMATIC BRIDGING MUSIC. FADE AND HOLD UNDER</u>**

**<u>Scene 6. At the Omer's</u>**

**Hassan**

**73. HASSAN:** *(crying softly to himself)* **Mama, kwanini uliniacha . Nataka kuwa na wewe** ***(sobs then sounding more determined)*** **Wakubwa zangu kwenye Madrassa wanasema kuwa naweza kuungana nawe peponi iwapo nitajitolea mhanga dhidi ya makafiri. Wakristo wanatupiga vita, kupinga ujenzi wa msikiti….! Mama nataka kuwa na wewe** ***(Sobs)***

**<u>MUSIC FADE</u>**

**<u>Scene7. Under the bridge</u>**

**Harry, Layla**

**74. <u>SFX: Walking /normal traffic sounds, stepping down stony stairs, river flowing, birds singing</u>**

**75. HARRY:** **Twende huku , tufuate hizi ngazi.. Haahhh!** ***(sighs)*** **Huku chini ya Daraja ni kuzuri na kuna ubaridi. Unaweza kukalia koti langu.**

**76. LAYLA:** **Ahsante. Harry..!.**

**77. HARRY:** *(trying to find the right words)* **Layla – ummmmm.. kama ujuavyo,… ummm….familia zetu hazipendani kabisa!!**

**78. LAYLA:** Sikuelewi.

**79. HARRY:** **Ummmm ...Ni babangu mdogo. Amenikataza kukuona au kutembea nawe nje ya mazingira ya shule….**

**80. LAYLA:** **Kwanini Babako mdogo ananipinga… hanipendi.?**

**81. HARRY:** **Sio eti hakupendi wewe binafsi. Sikiliza, familia za Dembele na Omer zinahasimiana. Babangu anasema kuwa ni kwasababu ya ardhi.Waislamu wanataka kujenga msikiti kwenye ardhi hiyo.**

**82. LAYLA:** ***(angry)* Hapana..! Ni nyinyi mnaotaka kujenga kanisa katika ardhi hiyo..**

**83. HARRY:** **Na hilo ndilo tatizo. Unadhani tunaweza kulitafutia suluhu..?**

**84. LAYLA:** **Tunaweza… tusubiri uamuzi wa baraza la maendeleo.**

**85. HARRY:** ***(relieved)* Haswa!Hizo ndizo kauli zinazofaa.! Nilitaka tu… *(sighs)* labda sikujieleza vizuri…. Nilitaka kusema….**

**86. LAYLA:** ***(softer)*** Enhe,nini**?**

**87. HARRY:** ***(big sigh)*** **Nataraji suala hili halitauvuruga uhusiano wetu. Nakupenda sana Layla. Tumefahamiana kwa muda wa mwaka mmoja sasa, lakini..ummm…**...

**88. LAYLA:** ***(helping)*** **Nadhani naelewa unachokisema…! Pia mimi ningependa tujuane vizuri Harry!**

**89. HARRY:** ***(happier)*****Kweli? ...Ohhh Layla!** ***(desperate again)*** **Lakini je Familia zetu zikileta pingamizi?**

**90. SIG TUNE UP**

**91. OUTRO:**

**Na hadi hapo tunafika mwisho wa kipindi hiki cha Noa Bongo kwa leo. Layla na Harry wameamua kuipa kisogo mivutano baina ya familia zao.Hata hivyo wana kibarua kigumu.Ungana nasi tena kwenye sehemu ya 5 kwenye mfululizo wa mchezo huu wa Daraja la Mto Gori, wakati wa ufunguzi rasmi wa Kundi la mjadala na mdahalo unaosubiriwa kwa hamu kubwa.Pia utasikia habari za kushtua zinazotishia kusababisha sintofahamu katika penzi chipukizi la Harry na Layla.Kumbuka ukiwa na maoni au ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.!**

**END OF EPISODE 4**